



MASENO UNIVERSITY

UNIVERSITY EXAMINATIONS 2017/2018

**THIRD YEAR FIRST SEMESTER EXAMINATION FOR
THE DEGREE OF BACHELOR OF EDUCATION ARTS WITH
INFORMATION TECHNOLOGY**

MAIN CAMPUS

ECT 316: MBINU ZA KUFUNDISHWA KISWAHILI

Date: 23rd February, 2018

Time: 3.30 - 6.30pm

MAAGIZO:

- **Jibu swali la KWANZA na mengine MATATU**



SWALI LA KWANZA

- a) Fafanua shabaha za kufundisha Lugha na Fasihi katika shule za upili inavyoelezwa katika silabasi nchini Kenya. [Alama 5]
- b) Eleza sifa zitakazokutambua kama mwalimu bora wa lugha na fasihi. [Alama 5]
- c) Dhihirisha umuhimu wa Silabasi kama ala ya kufundishia. [Alama 5]
- d) Eleza shabaha tano za kufundisha fasihi. [Alama 5]
- e) Ni kwa njia gani unavyoweza kusahihisha makosa ya matamshi ya wanafunzi wako? [Alama 5]

SWALI LA PILI

- a) Onyesha umuhimu wa kutathmini ufahamu wa wanafunzi wako katika lugha na fasihi. [Alama 5]
- b) Jadili vipengele utakavyolenga unapopima insha za wanafunzi wako. [Alama 10]

SWALI LA TATU

- a) Fafanua dhana 'Uchambuzi wa maandishi ya Kifasihi.' [Alama 5]
- b) Ukizingatia riwaya uliyoisoma, jadili mambo utakayomshauri mwanafunzi wako kulenga anapochambua maandishi ya Fasihi. [Alama 10]

SWALI LA NNE

- a) Eleza umuhimu wa kushirikisha vifaa visaidizi katika ufundishaji wa lugha na fasihi. [Alama 5]
- b) Onyesha vigezo vitakavyokuongoza kutambua vitabu vifaavyo kufundishia Fasihi katika kidato cha kwanza. [Alama 10]

SWALI LA TANO

a) Kwa kutoa mifano mwafaka, eleza sababu zinazofanya ushairi kuonekana mgumu kwa wanafunzi wengi. [Alama 5]

b) Pendekeza namna ya kufanya ushairi kuwavutia wanafunzi wako.

[Alama 10]

SWALI LA SITA

Jadili matatizo yanayokumba ufundishaji wa lugha na Fasihi nchini Kenya huku ukipendekeza namna ya kuyatatua. [Alama 15]